

# MIONGOZO KWA WAZAZI NA WAELIMISHAJI KUHUSU ULINZI WA WATOTO MTANDAONI

## Shukrani

Miongozo hii imeandaliwa na Muungano wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU) na kikundi kazi cha waandishi wachangiaji kutoka kwa taasisi zinazoongoza zinazofanya kazi katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na pia katika masuala ya ulinzi wa watoto (mtandaoni) na imehusisha mashirika yafuatayo:

ECPAT International, mtandao wa Global Kids Online, Muungano wa Kimataifa wa Walemavu, Muungano wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU), Chuo cha London cha Uchumi na Sayansi ya Siasa, Internet Matters, Parent Zone International na UK Safer Internet Centres/SWGfL.Kikundi kazi kiliongozwa na Karl Hopwood (Mtandao wa Insafe wa Safer Internet Centres (Insafe) [1] na kuratibiwa na Fanny Rotino (ITU).

Michango ya thamani pia ilipokelewa na COFACE-Families Europe, Kamisheni ya jukwaa la Kielektroniki la eSafety la Australia, Kamisheni ya Ulaya, Baraza la Ulaya, Kundi la e-Worldwide (e-WWG), ICMEC, Vijana na Vyombo vya Habari/ Kituo cha Mtandao na Jamii cha Berkman Klein katika Chuo Kikuu cha Harvard pamoja na serikali za kitaifa na wadau wa sekta binafsi ambao wana lengo moja la kufanya Intaneti kuwa kitu bora na salama kwa watoto na vijana.

Miongozo hii isingewezekana bila muda, shauku na kujitolea kwa waandishi wachangizi.

ITU inawashukuru washirika wafuatao, ambao wametoa muda wao muhimu na maarifa (yaliyoorodheshwa kwa mpangilio wa alfabeti wa shirika husika):

- Julia Fossi and Ella Serry (Kamisheni ya Australian eSafety)
- Martin Schmalzried (COFACE-Families Europe)
- Livia Stoica (Baraza la Ulaya)
- John Carr (ECPAT International)
- Manuela Marta (Kamisheni ya Ulaya)
- Salma Abbasi (e-WWG)
- Laurie Tasharski (ICMEC)
- Lucy Richardson (Muungano wa Kimataifa wa Walemavu)
- Carolyn Bunting (Masuala ya Intaneti)
- Fanny Rotino (ITU)
- Sonia Livingstone (Chuo cha London cha Uchumi & Global Kids Online)
- Cliff Manning na Vicki Shotbolt (Parent Zone International)
- David Wright (Vituo vya Intaneti Salama vya Uingereza/SWGfL)
- Sandra Cortesi (Vijana na Vyombo vya Habari)

[1] *Chini ya Shirika la Connecting Europe Facility (CEF), European Schoolnet inaendesha, kwa niaba ya Kamisheni ya Ulaya, jukwaa la Better Internet for Kids ambalo linalojumuisha uratibu wa mtandao wa Insafe wa Vituo vya Intaneti Salama Ulaya. Maelezo zaidi yanapatikana katika*
www.betterinternetforkids.eu

**ISBN**

© ITU 2020

Baadhi ya haki zimehifadhiwa. Kazi hii imepewa leseni kwa umma kupitia leseni ya Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 3.0 IGO (CC BY-NC-SA 3.0 IGO).

Chini ya masharti ya leseni hii, unaweza kunakili, kusambaza upya na kurekebisha kazi hii kwa malengo yasiyo ya kibiashara, kwa kuwa marejeleo yametajwa ipasavyo. Katika matumizi yoyote ya kazi hii, kusiwe na pendekezo kwamba ITU inaunga mkono shirika, bidhaa au huduma zozote mahususi. Matumizi yasiyoidhinishwa ya majina au nembo za ITU hayaruhusiwi. Ukiikubali kazi, basi ni lazima uikatie leseni chini ya leseni sawa au inayolingana ya Creative Commons. Ukitafsiri kazi hii, unapaswa kuongeza kanusho lifuatalo pamoja na nukuu iliyopendekezwa ya: "Tafsiri hii haikufanywa na Muungano wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU). ITU haiwajibikii maudhui au usahihi wa tafsiri hii. Toleo la asili la Kiingereza litakuwa toleo la kisheria na la kweli". Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea

https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/3.0/igo/

## Dibaji

ITU ilibuni jozi yake ya kwanza kabisa ya Miongozo ya Ulinzi wa Mtoto Mtandaoni mwaka wa 2009. Lengo letu hapo awali lilikuwa kutoa mfumo unaokubaliwa kimataifa kwa wadau mbalimbali - wazazi na waelimishaji, tasnia, watunga sera na watoto - ili kuwaweka salama watumiaji wa Intaneti wa umri mdogo zaidi, kwa furaha na kujiamini wanapotumia mtandao.

Tangu wakati huo, mtandao umebadilika zaidi ya ulivyokuwa. Imekuwa nyenzo kuu zaidi kwa watoto, inayotoa michezo ya kielimu, shughuli za kufurahisha, na njia nyingi tofauti za kusambaza habari, kujifunza, na kutangamana na marafiki, familia na ulimwengu wa nje. Lakini wakati huo huo, imekuwa mahali hatari zaidi kwa watoto wanapoitumia bila uangalizi.

Kuanzia masuala ya faragha, habari feki na za uwongo, hadi kwa mambo yenye vurugu na yasiyofaa, walaghai kupitia Intaneti, na wazushi wa utapeli mtandaoni na unyanyasaji wa kingono na dhuluma kwa watoto - na walezi wao - wanakabiliwa na hatari na changamoto nyingi.

Kwa kuongezea, janga la UVIKO-19 lilishuhudia kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaojiunga na ulimwengu wa mtandaoni kwa mara ya kwanza, ili kuwasaidia kimasomo na kudumisha mwingiliano wao kijamii. Vikwazo vilivyoletwa na virusi hivyo havikumaanisha tu kwamba watoto wengi wa umri mdogo walianza kutumia mitandao mapema zaidi kuliko walivyokadiria wazazi wao, lakini hitaji la kushughulikia majukumu ya kazi liliwaacha wazazi wengi kushindwa kuwaangalia watoto wao, na kuwaacha watoto katika hatari ya kutazama mambo yasiyofaa au kulengwa na wahalifu katika utengenezaji wa filamu za ngono za watoto.

Kwa kutambua hili, Nchi Wanachama za ITU ziliomba kitu zaidi ya Miongozo ya COP ambayo tumekuwa tukitekeleza mara kwa mara huko nyuma. Badala yake, miongozo hii mipya iliyosahihishwa imefikiriwa upya, kuandikwa upya na kusanifiwa upya kuanzia chini hadi juu, ili kuakisi mabadiliko makubwa sana katika mifumo ya kidijitali ambamo watoto wa leo wanajikuta.


Kwenu nyinyi, watumiaji wa miongozo hii, lengo letu limekuwa kutoa hamasisho la kina kuhusu changamoto, na kuwapa nyenzo ambayo itawasaidia kuunga mkono kwa ufanisi mwingiliano wa vijana na ulimwengu wa mtandaoni. Miongozo hii itakufahamisha kuhusu hatari na vitisho vinavyoweza kutokea, na kukusaidia kukuza mazingira salama na wezeshi ya mtandao nyumbani, na darasani. Pia inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi na mazungumzo yanayoendelea na watoto, ili kuunda nafasi salama ambapo watumiaji wa umri mdogo watahisi kuwezeshwa kutoa lalama zao.

Kando na kuakisi maendeleo mapya katika teknolojia na majukwaa ya kidijitali, toleo hili jipya linaziba pengo muhimu, yaani: hali inayowakabili watoto wenye ulemavu, ambao ulimwengu wa mtandaoni huwapa njia muhimu ya maisha kwa ukamilifu - na kuwatimizia – ushirikishwaji kijamii. Uzingatiaji wa mahitaji maalum ya watoto wahamiaji na makundi mengine yaliyo hatarini pia umejumuishwa.

Kutokana na msukumo halisi wa ITU kama mratibu wa kimataifa, ninajivunia ukweli kwamba miongozo hii iliyorekebishwa ni zao la juhudi za ushirikiano wa kimataifa, baada ya kuandikwa na wataalamu kutoka kwa jumuiya pana ya wadau mbalimbali.

Nina furaha pia kutambulisha kinyago chetu kipya cha COP, Sango, chenye urafiki, kichangamfu na jasiri kilichoundwa kabisa na kundi la watoto wenyewe, kama sehemu ya programu mpya ya kimataifa ya ITU ya kuwafikia vijana.

Katika enzi ambapo vijana wengi zaidi wanazuru mitandao, miongozo hii ya COP ni muhimu zaidi kuliko hapo awali. Wazazi na waelimishaji, tasnia, watunga sera - na watoto wenyewe - wote wana jukumu muhimu katika usalama wa watoto mitandaoni. Natumai utapata miongozo hii kuwa ya msaada unapoandamana na watoto unaowalea kwenye safari hii ya ajabu utakayogundua fursa tele kutoka kwa intaneti.



Doreen Bogdan-Martin

Mkurugenzi, Ofisi ya Maendeleo ya Mawasiliano

## Yaliyomo

Miongozo kwa wazazi na waelimishaji kuhusu ulinzi ........ 1
Shukrani ........ 1
ISBN ........ 2
Dibaji ........ 3
Muhtasari wa kiutendaji ........ 7
Utangulizi ........ 9
2. Ulinzi wa watoto mtandaoni ni nini ? ........ 12
3. Watoto na vijana katika ulimwengu uliounganishwa ........ 13
4. Watoto walio katika hali hatarishi ........ 29
5. Hatari na changamoto mpya zinazoibuka ........ 33
6. Kuelewa hatari na madhara ........ 41
7. Jukumu la wazazi, watunzaji na walezi ........ 47
8. Miongozo kwa wazazi, watunzaji na walezi ........ 51
9. Jukumu la waelimishaji ........ 58
10. Miongozo kwa waelimishaji ........ 65

## Vielelezo

Kielelezo cha 1: Watoto (%) wanaocheza michezo ya mtandaoni angalau kila wiki kulingana na....... 15

Kielelezo cha 2: Watoto (%) wanaofanya shughuli tatu au zaidi za kijamii mtandaoni angalau .......... 17

Kielelezo cha 3: Watoto (%) ambao hufanya angalau shughuli moja ya ubunifu mtandaoni .............. 19

Kielelezo cha 4: Watoto (%) ambao hufanya shughuli tatu au zaidi za kutafuta habari angalau ......... 21

Kielelezo cha 5: Watoto (%) ambao wamepata madhara mtandaoni, kulingana na jinsia na ............. 25

Kielelezo cha 6: Watoto (%) wanaotumia Intaneti nyumbani angalau kila wiki, kulingana na jinsia na ........................................................................................................................................................... 28

Jedwali 1: Vipengee muhimu vya kuzingatia kwa wazazi, watunzaji na walezi .................................. 51

Kielelezo cha 8: Watoto wakisema iwapo wamepewa taarifa au ushauri wowote kuhusu jinsi ......... 60

## Muhtasari wa kiutendaji

Kulingana na takwimu za ITU, kulikuwa na wastani wa watu bilioni 4.1 wanaotumia Intaneti mwaka wa 2019, likiwa ongezeko la asilimia 5.3 ikilinganishwa na makadirio ya 2018.

Watoto na vijana hutumia Intaneti kwa madhumuni mbalimbali, kuanzia kupata taarifa za mradi wa shule hadi kusema na marafiki. Wana ujuzi wa hali ya juu katika kusimamia apu na programu changamano, kuunganisha kwenye intaneti wakitumia simu za mkononi, tableti na vifaa vingine vya mkononi kama vile saa, iPod Touch, visoma-vitabu kielektroniki na vifaa vya michezo ya mitandaoni. [2]

Mtandao pia umetumika kama nyenzo muhimu katika maisha ya makundi mbalimbali ya watoto na vijana walio katika mazingira magumu. Watoto wahamiaji huutumia kudumisha uhusiano na familia na marafiki na huwapa fursa ya kushiriki utamaduni wao mpya. Huwawezesha watoto na vijana wenye ulemavu kushirikiana na kuhusika katika shughuli ambazo hazipatikani nje ya mtandao, na hutoa fursa za kuwa katika hali sawa na wenzao mtandaoni, wenye uwezo unaoonekana zaidi kuliko ulemavu.

Hata hivyo, pamoja na kuwa intaneti ina fursa anuwai kama hizi, pia huwa na hatari na madhara, baadhi ya watumizi wakiwa katika hatari zaidi kuliko wengine. Kwa mfano, kwa watoto na vijana wanaohama makwao, matokeo ya ukiukaji wa taarifa za siri mtandaoni yanaweza kuwa makubwa – ikiwa mikononi mwa watu wasiofaa, data inaweza kutumika kuwatambua na kuwalenga watu kulingana na makabila yao, hali ya uhamiaji, au viashiria vingine vya utambulisho wao[3] ; kwa watoto na vijana walio na ugonjwa wa tawahudi (ASD), changamoto za kijamii kama vile ugumu wa kuelewa nia za wengine, zinaweza kuacha kundi hili katika hatari ya "marafiki" wenye nia mbaya; na watoto na vijana wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa wa kutengwa, kunyanyapaliwa, na kudanganywa.

Wazazi na walezi wengi huwa na dhana potofu kwamba mtoto wao yuko salama zaidi ikiwa anatumia kompyuta nyumbani, au shuleni, kuliko mahali pengine. Hii ni dhana potofu na hatari kwa sababu Intaneti inaweza kuwafikisha watoto na vijana mahali popote duniani, na kwa hali hiyo, wanaweza kukabiliwa na hatari zinazoweza kuwavuruga mno, kama iwapo wangekuwa katika ulimwengu halisi. Hata hivyo, watoto na vijana hukabiliwa na ongezeko la hatari ya kudhuriwa wanapoingia mitandaoni kupitia simu za kisasa, tableti au vifaa vingine vya mkononi. Hii ni kwa sababu ni rahisi na ni haraka sana kuingia mtandaoni wakitumia vifaa hivi vya mkononi kutoka mahali popote na vina uwezekano mdogo wa kufuatiliwa na wazazi au walezi.

Miongozo hii imetengenezwa kwa kuzingatia mpango wa ulinzi wa watoto katika mitandao (COP), kama sehemu ya Agenda ya Kiulimwengu ya ITU ya Kukabili Uhalifu Kimtandao[4], kwa

---

[2] ITU, (2019), Measuring digital development. Facts and figures 2019, *https://www.itu.int/en/ITU-D/Statistics/Documents/facts/FactsFigures2019.pdf*.

[3] UNICEF (2017), *The State of the World's Children 2017: Children in a Digital World,* *https://www.unicef.org/uzbekistan/media/711/file/SOWC:%20Children%20in%20a%20Digital%20World.pdf*.

[4] ITU (2020), *Global Cybersecurity Agenda (GCA)*, *https://www.itu.int/en/action/cybersecurity/Pages/gca.aspx.*

lengo la kuweka misingi ya matumizi salama ya intaneti si tu kwa vijana wa kisasa bali pia kwa vizazi vijavyo. Miongozo hii pia inalenga watoto walio katika mazingira magumu, hasa, watoto wahamiaji, wanaougua ASD na watoto wenye ulemavu.

Miongozo hiyo inakusudiwa kufanya kazi kama kielelezo ambacho kinaweza kubadilishwa na kutumiwa kwa njia inayoambatana na mila na desturi za kitaifa au za mitaa na kushughulikia masuala ambayo yanaweza kuathiri watoto na vijana wote walio chini ya umri wa miaka 18.

Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto unamfafanua mtoto kuwa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18. Miongozo hii inashughulikia masuala yanayowakabili watu wote walio chini ya umri wa miaka 18 katika sehemu zote za dunia. Hata hivyo, hakuna uwezekano mkubwa kwa mtumiaji wa Intaneti wa umri mdogo wa miaka saba kuwa na mahitaji au maslahi sawa na mtoto mwenye umri wa miaka 12 anayeanza Shule ya Upili au mwenye umri wa miaka 17 anayekaribia utu uzima. Miongozo hii imeundwa ili kutoa ushauri au mapendekezo kwa miktadha tofauti kwa sababu mahitaji mahususi yanahitaji kuzingatiwa kwa mtu binafsi na kwa sababu vipengele tofauti vya eneo, sheria na utamaduni vina mchango muhimu kuhusu jinsi miongozo hii inaweza kutumika au kufasiriwa katika nchi au eneo husika.

## Utangulizi

Katika kiwango cha kimataifa, mtumiaji mmoja kati ya watatu wa Intaneti ni wa chini ya umri wa miaka 18[5], kiwango cha kushangaza kutokana na kwamba katika 2018, zaidi ya nusu ya watu duniani walitumia Intaneti. Katika nchi zinazoendelea, watoto wanaongoza kwa matumizi ya Intaneti, wamekua wakitumia Intaneti kwenye simu zao kwanza. [6]

Huku watoto wengi zaidi duniani wakiendelea kufikia huduma za intaneti mtandao, kuzingatiwa kwa haki zao kutachangiwa zaidi na kile kinachotokea mtandaoni. Ufikiaji wa intaneti ni msingi wa utambuzi wa haki za watoto.

Ingawa mtoto mmoja kati ya watatu huweza kutumia Intaneti, bado kuna takriban watoto milioni 346 duniani kote ambao hawajaunganishwa kwenye mtandao[7]. Wale ambao wanaweza kufaidika zaidi na fursa ambazo mtandao hutoa mara nyingi ndio ambao hawajaunganishwa sana. Tunaona kuwa katika kanda ya Afrika karibu asilimia 60 ya watoto hawapati huduma za intaneti, ikilinganishwa na asilimia 4 barani Ulaya.[8]

Kuhusu uwezo wa kufikia mtandao, tofauti kubwa ipo pia kwa misingi ya jinsia. Utafiti[9] unaonyesha kuwa katika kila eneo isipokuwa Amerika, watumiaji wa mtandao wanaume ni wengi kuliko watumiaji wa kike. Katika nchi nyingi, wasichana hawana fursa sawa za kufikia mtandao kama wavulana, na hata pale wanapopata, wasichana mara nyingi hufuatiliwa na kuwekewa vikwazo katika matumizi yao ya mtandao kwa kiwango kikubwa zaidi.

Mgawanyiko wa kidijitali hukiuka uwezo wa ufikiaji. Watoto wanaotegemea simu za mkononi badala ya kompyuta wanaweza kupata tu uzoefu wa pili bora wa mtandaoni, na wale ambao hawana ujuzi wa kidijitali au kuzungumza lugha za wachache mara nyingi hawawezi kupata mambo muhimu mtandaoni. Kuna uwezekano mkubwa kwamba watoto kutoka maeneo ya vijijini wanaweza kuibiwa nywila au pesa. Pia huwa na ujuzi wa kiwango cha chini wa kidijitali, hutumia muda mwingi mtandaoni (hasa kucheza michezo), na hupokea maelekezo na ufuatiliaji mdogo wa wazazi . [10]

Watoto na watu wazima wanaripoti kuwa mgawanyiko wa kidijitali ni suala linaloendelea na linahitaji uwekezaji wa kujitolea na suluhu za kiubunifu. Katika hali kama hii, watoto wanafurika mitandaoni lakini wengi hawanufaiki na miongozo ifaayo kutoka kwa wazazi, walimu na watu wengine muhimu. Hii inaendelea kuwaweka watoto katika hatari.

Intaneti imeibuka kuwa teknolojia wezeshi na yenye ukwasi mkubwa. Watoto na vijana wamekuwa wanufaika wakuu wa Intaneti na teknolojia zinazohusiana na dijitali. Teknolojia hizi zinabadilisha jinsi tunavyowasiliana na zimefungua njia nyingi mpya za kucheza michezo,

---

[5] Livingstone, S., Carr, J., and Byrne, J. (2015) *One in three: The task for global internet governance in addressing children's rights*. Global Commission on Internet Governance: Paper Series. London: CIGI and Chatham House, https://www.cigionline.org/publications/one-three-internet-governance-and-childrens-rights

[6] ITU (2020), *Measuring the Information Society Report*, *https://www.itu.int/dms_pub/itu-d/opb/ind/D-IND-ICTOI-2018-SUM-PDF-E.pdf.*

[7] UNICEF (2017), *The State of the World's Children 2017: Children in a Digital World,* *https://www.unicef.org/uzbekistan/media/711/file/SOWC:%20Children%20in%20a%20Digital%20World.pdf*.

[8] UNICEF.

[9] Araba Sey and Nancy Hafkin (2019), *REPORT OF EQUALS RESEARCH GROUP, LED BY THE UNITED NATIONS UNIVERSITY (United Nations University and EQUALS Global Partnership),* *https://i.unu.edu/media/cs.unu.edu/attachment/4040/EQUALS-Research-Report-2019.pdf.*

[10] UNICEF (2019). *Growing up in a connected world*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence, https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20Summary%20Report.pdf.

kufurahia muziki na kushiriki katika safu kubwa ya shughuli za kitamaduni, na kuondoa vizuizi vingi. Watoto wanaweza kupanua wigo wao mtandaoni, kwa kutumia fursa za kukusanya taarifa na kukuza mahusiano. TEHAMA huwapa watoto ujuzi wa kusoma na kuandika ambao hukuza aina nyinginezo za ushiriki nje ya mtandao. Intaneti ni jukwaa mwafaka la ufikiaji wa masuala ya afya, huduma za elimu, na habari kuhusu mada ambazo ni muhimu kwa vijana lakini zinaweza kuwa mwiko katika jamii zao. Watoto na vijana mara nyingi sana wamekuwa mstari wa mbele katika kupatiliza na kutumia fursa ziletwazo na Intaneti.

Hata hivyo, ni jambo lisilopingika kwamba intaneti imeleta changamoto kadhaa kwa usalama wa watoto na vijana, ambazo zinahitaji kushughulikiwa, kwa sababu ni muhimu kwa haki zao wenyewe lakini pia kwa sababu ni muhimu kwa mawasiliano na kila mtu anayefahamu kwamba intaneti ni chombo cha kuaminika. Vile vile, ni muhimu kujua kwamba haja ya kulinda watoto na vijana mtandaoni haipaswi kuchukuliwa kuwa ni jukwaa la kuhalalisha shambulio la uhuru wa kujieleza, uhuru wa kutagusana au uhuru wa kujumuika.

Ni muhimu sana kwamba kizazi kijacho kitumie intaneti kwa kujiamini ili baadaye kiweze kuendelea kunufaika na mabadiliko yake. Hivyo, tunapojadili usalama wa watoto na vijana mtandaoni, ni muhimu kuwa na usawazisho unaofaa.

Ni muhimu kujadili kwa uwazi hatari zilizopo kwa watoto na vijana mtandaoni, kuwafundisha jinsi ya kutambua hatari, na kuzuia au kukabiliana na madhara iwapo yatatokea, bila ya kuwatisha au kuwaweka katika hali hatarishi zaidi.

Ni vigumu sana kwa watoto na vijana kuchukulia kwa uzito mbinu yoyote yenye miegemeo hasi katika kushughulikia suala la teknolojia. Wazazi na walimu mara nyingi wanaweza kujikuta katika hali mbaya kwa sababu mara nyingi vijana hujua zaidi kuhusu teknolojia na fursa zake kuliko vizazi vya zamani. Utafiti umeonyesha kuwa watoto wengi wanaweza kutofautisha unyanyasaji wa mtandaoni na utani au dhihaka za mtandaoni, wakitambua kwamba unyanyasaji wa mtandaoni unalenga kudhuru. Katika sehemu nyingi za dunia, watoto wana uelewa mzuri wa baadhi ya hatari wanazokabiliana nazo mtandaoni. [11]

Hata hivyo, ingawa inaweza kugunduliwa kuwa juhudi za kuwaelimisha watoto kukabiliana na hatari za mtandaoni zinazaa matunda, bado kuna haja ya kuongeza ufahamu wa watoto wengi zaidi duniani kote, hasa miongoni mwa makundi yaliyo hatarini, na sharti juhudi za pamoja zilenge watoto hawa hasa, ili kuboresha ufahamu wa huduma za usaidizi kwa waathiriwa wa unyanyasaji wa mtandaoni na aina zingine za hatari za mtandaoni.

Kuna changamoto nyingi zinazokuja. Matatizo hayaletwi na kufikia huduma za mtandaoni pekee kwa ulimwengu. Kiwango cha mabadiliko ya kiteknolojia kinaleta changamoto kwa usalama wa watoto mtandaoni. Watoto wengi hupitia mandhari changamano ya kidijitali. Maendeleo ya akili bandia na ujifunzaji wa mashine, uhalisia pepe na ulioboreshwa, data kubwa, utambuzi wa

[11] Tangu 2016, ITU imekuwa ikifanya mashauriano katika COP na wadau watoto na watu wazima kuhusu masuala muhimu kama unyanyasaji wa mtandaoni, kusoma na kuandika kidijitali na shughuli za watoto mtandaoni.

uso, robotiki na Intaneti ya Mambo imewekwa ili kubadilisha mitazamo ya utendaji wa watoto hata zaidi.

Ni muhimu kwamba wadau wote wapange na kuwazia kuhusu matokeo ya maendeleo haya kwa watoto na kutafuta njia za kuwaunga mkono ili kukuza ujuzi wa kidijitali unaohitajika sio tu kuishi bali kustawi katika siku zijazo za kidijitali. Uwekezaji zaidi katika ujuzi wa kidijitali na ujuzi wa kusoma na kuandika wa wazazi na walimu unahitajika ili kusaidia watoto kukuza fikra makini na ustadi wa kutathmini ili kuwawezesha kuelewa mtiririko wa haraka wa taarifa za ubora tofauti kutoka kwa wazazi na waelimishaji hadi watoto, yaani tuwe na raia waliobobea kidijitali. [12]

Utafiti wa ITU umeonyesha kuwa baadhi ya nchi zinatatizika kutenga rasilimali za kutosha kushughulikia ujuzi wa kidijitali na usalama wa watoto mtandaoni. Hata hivyo, watoto wanaripoti kuwa wazazi, walimu, kampuni za teknolojia na serikali zote ni wahusika muhimu katika kuandaa suluhu za kusaidia usalama wao mtandaoni. Utafiti wa ITU katika Nchi Wanachama unaonyesha kuwa kuna usaidizi mkubwa wa ushirikishwaji wa maarifa ulioimarishwa na juhudi zilizoratibiwa ili kulinda usalama wa idadi kubwa ya watoto mtandaoni.

Usawazishaji wa fursa na hatari za mtandaoni za watoto bado ni changamoto. Nchi Wanachama wa ITU pia zilionyesha kuwa ingawa ni lazima juhudi za kukuza fursa kwa watoto mtandaoni ziendelee kupewa kipaumbele, zinahitaji zisawazishwe kwa uangalifu na haki za hali salama ambapo wanaweza kushiriki na kufaidika na ulimwengu wa kidijitali. [13]

[12] Council of Europe (2016), *Digital Citizenship Education*, *https://www.coe.int/en/web/digital-citizenship education/home*.

[13] ITU News (2018), *Celebrating 10 Years of Child Online Protection*, *https://news.itu.int/celebrating-10-years-child-online-protection/.*

## 2. Ulinzi wa watoto mtandaoni ni nini ?

Teknolojia za mtandaoni huunda nafasi nyingi kwa watoto na vijana kuwasiliana, kujifunza ujuzi mpya, kuwa wabunifu na kuchangia katika kuboresha maendeleo ya jamii. Lakini pia wanaweza kuibua hatari mpya kama vile kufichuliwa shughuli zao za faragha, kupata mambo yanayokiuka sheria, uchokozwaji, unyanyasaji wa mtandaoni, matumizi mabaya ya data ya kibinafsi, mitindo ya uvaaji na hata unyanyasaji wa kingono kwa watoto.

Mwongozo huu unakuza mbinu pana ya kukabiliana na matishio na madhara yote ambayo watoto na vijana wanaweza kukumbana nayo wanapopata ujuzi wa kidijitali. Wanatambua kwamba wadau wote wanaohusika wana jukumu la kuimarisha maarifa yao kidijitali, ustawi na ulinzi huku wakinufaika na fursa ambazo Intaneti inaweza kutoa.

Kulinda watoto ni jukumu la kawaida na ni juu ya wadau wote wanaohusika kuhakikisha mustakabali endelevu kwa wote. Ili hilo lifanyike, ni sharti watunga sera, sekta ya kibinafsi, wazazi, walezi, waelimishaji na wadau wengine wahakikishe kwamba watoto wanajiwezesha ipasavyo - mtandaoni na nje ya mtandao.

Wazazi, walezi na waelimishaji pia wana wajibu wa kuhakikisha kwamba watoto na vijana wanatumia tovuti za Intaneti kwa usalama na kwa uwajibikaji.

Katika miaka ya hivi majuzi, ufikiaji wa intaneti kwenye simu za mkononi umeongezeka sana na hakuna suluhu bainifu ya kulinda watoto na vijana dhidi ya hatari za mtandao. Hili ni suala la kimataifa ambalo linahitaji mwitikio wa kimataifa kutoka kwa sekta zote za jamii, ikiwa ni pamoja na watoto na vijana wenyewe.

Ili kukabiliana na changamoto hizi zinazoongezeka katika kukabiliana na maendeleo ya haraka ya TEHAMA, Mpango wa Ulinzi wa Mtoto Mtandaoni (COP) [14], mpango wa kimataifa wa wadau mbalimbali uliozinduliwa na ITU mwezi Novemba 2008, unaendelea kuleta washirika pamoja kutoka sekta zote dunia ni ili kuunda matumizi salama na yenye kuwezesha mtandaoni kwa watoto na vijana duniani kote. Inaweka miongozo kwa wadau wote husika, wakiwemo watoto na vijana katika sehemu zote za dunia kuhusu jinsi ya kujiweka salama mtandaoni. Mwongozo huu ni kama kilelezo ambacho kinaweza kubadilishwa na kutumika kwa njia ambayo inalingana na desturi na sheria za kitaifa au za mitaa husika.

Ripoti hii imetayarishwa ndani ya Mpango wa COP na kikundi kazi cha wataalamu wa wadau mbalimbali na inalenga kutoa maelezo, ushauri na vidokezo muhimu vya usalama kwa wazazi, walezi na waelimishaji kuhusu ulinzi wa watoto mtandaoni.

Kikundi kazi cha wataalamu wa ITU kiliandika kwa pamoja miongozo katika ripoti hii, kikijalizia kwenye Mwongozo wa kwanza wa ITU COP, uliotolewa mwaka wa 2009 na kusasishwa mwaka wa 2016. Kuhusu ombi la Nchi Wanachama wa ITU, ITU ilizindua mchakato wa ukaguzi mwaka 2019 ambao ulilenga kuunda toleo la pili la miongozo.

Miongozo hii mipya inashirikisha hali maalum ya watoto wenye ulemavu kuhusiana na hatari na madhara ya matumizi ya mtandao pamoja na masuala yanayohusu maendeleo ya teknolojia mpya kama vile Intaneti ya simu ya mkononi, programu, Mtandao wa Mambo, vifaa vya kuchezea vilivyounganishwa intaneti, michezo ya mitandaoni, robotiki, mashine za kujifunza, na akili ya bandia.

[14] ITU (2020), *Child Online Protection*, *https://www.itu.int/en/cop/Pages/default.aspx*.

## 3. Watoto na vijana katika ulimwengu uliounganishwa[15]

Katika ngazi ya kimataifa, imekadiriwa kuwa mtoto mmoja kati ya watatu ni mtumiaji wa Intaneti na kwamba mtumiaji mmoja kati ya watatu wa Intaneti ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18[16]. Mnamo 2017, nusu ya idadi ya watu duniani walitumia mtandao; katika kikundi cha umri wa miaka 15 hadi 24, idadi iliongezeka hadi karibu thuluthi mbili.

"Tulikua tukitumia intaneti. Ninamaanisha, Intaneti imekuwa hapa nasi kila wakati. Utasikia watu wazima wakimaka 'Alaa Intaneti imeonekana', wakati ni jambo la kawaida kwetu." - Mvulana, miaka 15, Serbia

Kifaa maarufu zaidi cha kufikia intaneti miongoni mwa watoto na vijana ni simu ya mkononi. Hii inawakilisha mabadiliko muhimu katika muongo mmoja uliopita. Huko Ulaya na Amerika Kaskazini, kizazi cha kwanza cha watumiaji wa Intaneti waliingia kupitia kompyuta ya mezani, lakini mwelekeo katika nchi nyingi zinazoendelea umekuwa kupitia simu za mkononi 'kwa mara ya kwanza'.

Watoto na vijana wanapendelea kutumia simu za mkononi kwa sababu wanaweza kuzibeba kila mahali; si lazima kutumia pamoja na jamaa zao wengine; inaweza kukidhi haja zao kadhaa kwa wakati mmoja, kama vile kutuma jumbe, kuzungumza, kubofya na kutuma picha, na kuvinjari; na huwashwa kila wakati.

"Simu ni rahisi kwa namna fulani. Tunaweza kubeba popote, ni ndogo na ni rahisi kuifanyia kazi. Ninaipenda zaidi kwa njia hii [ninapoitumia] kwa vidole na sio kwa kibodi. Msichana wa miaka 12, Serbia

Tafiti zimeonyesha kuwa miongoni mwa watoto na vijana wanaoweza kufikia Intaneti, wasichana na wavulana wana viwango sawa vya matumizi ya simu za mkononi kuingia mtandaoni. Kwa kulinganisha, kompyuta za mezani hutumiwa zaidi na wavulana.

Kiuhalisia, watoto na vijana wengi wanapata Intaneti kupitia kifaa kimoja au zaidi na kuna tabia ya wavulana kutumia vifaa vingi kuliko wasichana katika kila nchi iliyofanyiwa utafiti.

---

[15] This chapter is mainly drawn from the following source: UNICEF (2019). *Growing up in a connected world*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence: - https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20Summary%20Report.pdf .
The comprehensive research, as part of the comparable high-quality evidence work of the Global Kids Online, collects voices from children in 11 countries, across 4 regions, from 2016 to 2018 (14,733 children aged 9-17 years). The report focuses at the positive effects of ICTs for children and asks at the same time when the use of ICTs becomes problematic in children's lives. All figures of chapter 4 here below are taken from this report. Qualitative and quantitative methodology on which these findings are based can be found at Livingstone, S., Kardefelt Winther, D., and Saeed, M. (2019). *Global Kids Online Comparative Report, Innocenti Research Report*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence. Online under: https://www.unicef-irc.org/publications/1059-global-kids-online-comparative-report.html Further information on the Global Kids Online international research project can be found online under: http://globalkidsonline.net.

[16] Livingstone, S., Carr, J., and Byrne, J. (2015) *One in three: The task for global internet governance in addressing children's rights*. Global Commission on Internet Governance: Paper Series. London: CIGI and Chatham House, https://www.cigionline.org/publications/one-three-internet-governance-and-childrens-rights

Watoto na vijana hutumia wastani wa saa mbili kwa siku mtandaoni katika wiki na takribani mara mbili ya ile kila siku ya wikendi. Wengine wanahisi wameunganishwa kabisa. Lakini wengine wengi bado hawana ufikiaji wa Intaneti nyumbani - au wana ufikiaji uliodhibitiwa.

Hata hivyo, takwimu hutofautiana sana na kuna maoni mbalimbali kuhusu muda ambao watoto hutumia mtandaoni. Baadhi ya utafiti wa hivi majuzi kutoka Taasisi ya DQ unapendekeza kuwa nchini Australia watoto na vijana wanaweza kuwa wakitumia muda wa saa 38 kwa wiki mtandaoni. [17]

"Ninaenda kwenye mkahawa kwa sababu hatuna kompyuta nyumbani.... Hatuwezi kupata Intaneti shuleni." Mvulana, mwenye umri wa miaka 15-17, Afrika Kusini

"[Nimeunganishwa] Siku nzima, lakini sio kwamba ninaitumia siku nzima." Mvulana, mwenye umri wa miaka 13-14, Argentina.

Licha ya matokeo ya Global Kids Online (GKO) kwamba idadi sawa ya jumla ya wasichana na wavulana wanaweza kupata Intaneti, hata hivyo, katika baadhi ya nchi, wavulana wana uhuru zaidi wa matumizi ya Intaneti kuliko wasichana na kwamba wasichana mara nyingi hufuatiliwa na kuwekewa vikwazo katika maisha yao na matumizi yao ya Intaneti kudhibitiwa.

### Ulimwengu wa starehe

Watoto na vijana mara nyingi huenda mtandaoni kwa sababu mbalimbali chanya na za kuwafurahisha. Katika nchi 11 zilizofanyiwa utafiti, shughuli maarufu zaidi - kwa wasichana na wavulana - ni kutazama klipu za video. Zaidi ya robo tatu ya watoto na vijana wanaotumia Intaneti wanasema wanatazama video mtandaoni angalau kila wiki, ama wakiwa peke yao au pamoja na jamaa zao.

“Mama yangu aliponunua kipakatalishi, tulianza kutumia muda mwingi pamoja; kila wikendi tulichagua filamu na kuitazama na nyanya yangu.” Msichana, mwenye umri wa miaka 15, Uruguay.

Watoto na vijana pia hufurahia kucheza michezo mtandaoni, hivyo kutekeleza haki yao ya kucheza na wakati mwingine haki yao ya kujifunza. Kuna uwezekano mkubwa zaidi wa wavulana kucheza michezo ya mtandaoni katika nchi zote zilizochunguzwa. Hata hivyo, wasichana wengi wanaotumia Intaneti hucheza michezo ya mtandaoni; kwa mfano, wasichana wengi hucheza michezo ya mtandaoni nchini Bulgaria (60%) na Montenegro (80%). Kama ilivyo kwa kutazama video, kuna uwezekano mkubwa kwa watoto na vijana kucheza michezo ya mtandaoni wanapopata Intaneti kwa urahisi.


"Ninacheza michezo ya mtandaoni na kupata pesa kutoka kwayo." Mvulana, mwenye umri wa miaka 17, Ufilipino.


Watu wazima wana wasiwasi juu ya watoto na vijana kutumia muda mwingi kwenye skrini au huamini kwamba wanapoteza tu muda kwenye burudani ya mtandaoni. Kulingana na Global

[17] DQ Institute (2020), Child Safety Index, https://www.dqinstitute.org/child-online-safety-index/

Kids Online, shughuli hizi kuu za burudani zinaweza kutoa fursa muhimu kwa watoto na vijana, ambapo zinaweza kuwasaidia kukuza maarifa na ujuzi wa kuendelea zaidi katika masuala ya kielimu, kimawasiliano na kijamii mtandaoni.

**Kielelezo cha 1: Watoto (%) wanaocheza michezo ya mtandaoni angalau kila wiki kulingana na jinsia na umri [18]**




| | |
|---|---|
| Swali C4z-aa: Umecheza michezo ya mtandaoni mara ngapi ukiwa peke yako ama na watu wengine katika mwezi mmoja uliopita? Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti | Swali C4z-aa: Umecheza michezo ya mtandaoni mara ngapi ukiwa peke yako ama na watu wengine katika mwezi mmoja uliopita? Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti |

Kielelezo cha 1 kinaonyesha chati mbili za upau zinazoonyesha majibu ya uchunguzi wa matumizi ya Intaneti kwa watoto: Je, ni mara ngapi umecheza michezo ya mtandaoni peke yako ama na watu wengine katika mwezi uliopita? Chati moja inaonyesha mgawanyo wa matumizi kati ya wasichana na wavulana, huku wavulana wakiitumia zaidi katika kila tukio. Chati nyingine inaonyesha mgawanyo kwa kundi la umri. Hili haliko wazi, saba kati ya nchi kumi zilizoorodheshwa zinaonyesha kuwa kikundi cha watoto wa miaka 9-11 hucheza mara nyingi au zaidi kuliko vikundi vingine viwili (watoto wa miaka 12-14 na watoto wa miaka 15-17) .

Asili: UNICEF

## Kuunda miungano mipya


Intaneti, pamoja na zana zake za utumaji wa ujumbe wa papo hapo na mitandao ya kijamii, imekuwa mahali muhimu pa kukutania ambapo watoto na vijana wanaweza kutumia haki yao ya uhuru wa kujieleza kwa kuungana na marafiki na familia zao na watoto wengine na vijana wenye maslahi sawia. Katika nchi 11 zilizofanyiwa utafiti, watoto na vijana wengi wanaweza kuchukuliwa kama 'wajenzi wa jamii', kwa kuwa wanashiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii mtandaoni kila wiki - kama vile kuzungumza na marafiki na familia, kutumia zana mbalimbali za kutuma ujumbe na kuwasiliana na watu. ambao wana maslahi sawa na yao. Baadhi ya watoto pia wanaripoti kwamba wanaona ni rahisi kueleza uhalisi wao mitandaoni.

[18] Mchoro huu ulitolewa kwenye: UNICEF (2019). *Growing up in a connected world*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence, https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20Summary%20Report.pdf

"Ninaweza kuonyesha uhalisia wangu mtandaoni, hakuna sheria ... nina marafiki zaidi ya 5,000 mtandaoni". Mvulana anayejitambulisha kama shoga, mwenye umri wa miaka 15, Ufilipino

Mwingiliano wa kijamii kwa njia ya Mtandao pia huongezeka kulingana na umri kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mfano, baadhi ya tovuti za mitandao ya kijamii zina kikomo cha umri cha chini kabisa kwa watoto na vijana, kwa kawaida hupata uhuru zaidi kadiri ya umri unavyoongezeka.

**Kielelezo cha 2: Watoto (%) wanaofanya shughuli tatu au zaidi za kijamii mtandaoni angalau kila wiki, kulingana na jinsia [19]**




| | |
|---|---|
| Swali C4: Umefanya hizi shughuli za mitandao ya kijamii mtandaoni mara ngapi kwa mwezi uliopita? Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti | Swali C4: Umefanya hizi shughuli za mitandao ya kijamii mtandaoni mara ngapi kwa mwezi uliopita? Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti |

Kielelezo cha 2 kinaonyesha chati mbili za upau zinazoonyesha majibu ya uchunguzi wa matumizi ya Intaneti miongoni mwa watoto kwa shughuli za kijamii mtandaoni katika mwezi uliopita: Chati moja inaonyesha mgawanyo wa matumizi kati ya wasichana na wavulana, na matumizi sawa kwa wavulana na wasichana katika kila tukio isipokuwa moja. Chati nyingine inaonyesha mgawanyo kulingana na umri. Hii ilionyesha kuwa katika nchi zote zilizochunguzwa, kikundi cha watoto wa miaka 9-11 walitumia mtandao kwa shughuli za kijamii mtandaoni mara chache kuliko vikundi vingine viwili (watoto wa miaka 12-14 na 15-17), na kwa kila nchi, kundi la watoto wa miaka 15-17 walitumia zaidi.

Kumbuka: Watoto na vijana waliulizwa ni mara ngapi walifanya shughuli zifuatazo za kijamii mtandaoni katika mwezi uliopita: walitumia Intaneti kuzungumza na watu kutoka maeneo au malezi tofauti na yao; walizuru tovuti ya mtandao wa kijamii; walizungumza na familia au marafiki ambao waliishi mbali zaidi; walitumia ujumbe wa papo hapo; walizuru tovuti ambayo watu wabadilishana uzoefu wa mambo wanayopenda au uraibu wao.

Asili: UNICEF

Ni wazi kutokana na data iliyo hapo juu kwamba Intaneti hufungua nafasi mpya za kujumuika na watu, ingawa wazazi mara nyingi hulalamika kwamba mwingiliano wa watoto na vijana mtandaoni unasababishwa na mawasiliano ya kibinafsi katika ulimwengu halisi.

[19] Mchoro huu ulitolewa kwenye: UNICEF (2019). *Growing up in a connected world*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence, https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20Summary%20Report.pdf,

"Katika karamu, wameketi mezani. 10 kati yao kila mmoja ana kifaa chake kidogo." Mzazi wa matineja wa miaka 15-17, Chile

Tabia kama hiyo sio ya kipekee kwa watoto na vijana. Baadhi ya wazazi hupiga simu au kugandai mitandaoni wakati wa mikusanyiko ya kijamii - jambo ambalo hukera watoto na vijana wengi.

“Mezani, tunapokula, Baba anatumia simu yake. Huo ndio wakati pekee ambao sisi sote tuko pamoja, na inaniudhi sana.” Msichana, mwenye umri wa miaka 14, Uruguay

Kwa ufikiaji mkubwa wa Intaneti, watoto na vijana wanaweza kupanua wigo wao, kukusanya habari na kupanua mahusiano yao. Kwa mwingiliano zaidi wa kijamii, iwe mtandaoni au ana kwa ana, wao hujenga uzoefu na ujuzi wao. Utafiti wa GKO unaonyesha kuwa watoto na vijana wanaojumuika pakubwa kwenye Mtandao ni bora zaidi katika kudhibiti faragha yao ya mtandaoni, ambayo husaidia kuwaweka salama.

### Raha ya uundaji

Baadhi ya maudhui ya mtandaoni ambayo watoto na vijana hupata, na kuthamini yametolewa na watoto wengine na vijana. Kwa kawaida, katika nchi 11 zilizofanyiwa utafiti na Global Kids Online, asilimia 10 hadi 20 ya watoto na vijana huunda na kupakia video au muziki wao kila wiki, au kuandika blogu, au hadithi, au kuunda kurasa za wavuti kila wiki.


"Nina blogi na huisasisha mara kwa mara." Msichana, mwenye umri wa miaka 15-17, Ufilipino


"Unaweza kuweka video na michezo. Unaweza kuweka muziki. Unaweza pia kupakia picha, mawazo, michezo.” Msichana, mwenye umri wa miaka 9-11, Ghana

"Ninatengeneza kadi za DIY; Ninaziweka mtandaoni. Marafiki zangu wanazipenda.” Msichana, mwenye umri wa miaka 15-17, Ufilipino

"Ndio, najua jinsi ya [kudukua kompyuta], lakini sifanyi hivyo tena." Mvulana, mwenye umri wa miaka 15-17, Ufilipino

**Kielelezo cha 3: Watoto (%) ambao hufanya angalau shughuli moja ya ubunifu mtandaoni angalau kila wiki, kulingana na jinsia na umri [20]**




Question C4m–n: How often have you done creative activities online in the past month? Note: In Uruguay, children were not asked about creating blogs online. Base: All children who use the internet.

Question C4m–n: How often have you done creative activities online in the past month? Note: In Uruguay, children were not asked about creating blogs online. Base: All children who use the internet.

| | |
|---|---|
| Swali c4m-n: Je, umefanya shughuli za kiubunifu mara ngapi kwa mwezi mmoja uliopita? Kumbuka: Watoto hawakuulizwa kuhusu uundaji wa blogu mtandaoni katika Uruguay. Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti. | Swali c4m-n: Je, umefanya shughuli za kiubunifu mara ngapi kwa mwezi mmoja uliopita? Kumbuka: Watoto hawakuulizwa kuhusu uundaji wa blogu mtandaoni katika Uruguay. Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti. |

Kielelezo cha 3 kinaonyesha chati mbili za upau zinazoonyesha majibu ya uchunguzi wa matumizi ya Intaneti miongoni mwa watoto kwa shughuli za ubunifu mtandaoni katika mwezi uliopita: Chati moja inaonyesha mgawanyo wa matumizi kati ya wasichana na wavulana, na matumizi sawa ya ubunifu kwa wavulana na wasichana. Chati nyingine inaonyesha mgawanyo kulingana na umri. Hii ilionyesha kuwa katika nchi zote isipokuwa moja ya nchi zilizochunguzwa, kikundi cha watoto wa miaka 9-11 kilitumia mtandao kwa shughuli za ubunifu mtandaoni mara chache kuliko vikundi vingine viwili vya umri wa miaka (12-14 na 15-17) na kwa nchi zote ila moja ya nchi zilizochunguzwa, kikundi cha watoto wa miaka 15-17 walitumia zaidi intaneti kwa ubunifu.

Kumbuka: Watoto na vijana waliulizwa ni mara ngapi walifanya shughuli zifuatazo za ubunifu mtandaoni katika mwezi uliopita: walitengeneza video au muziki wao na kusambaza mtandaoni; kuunda blogi au simulizi au tovuti mtandaoni; video zilizochapishwa au muziki ulioundwa na mtu mwingine.

Asili: UNICEF

[20] Mchoro huu ulitolewa kwenye: UNICEF (2019). *Growing up in a connected world*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence, https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20Summary%20Report.pdf.

### Hamu ya habari

Kama watu wazima, watoto na vijana wanatumia mtandao kufurahia haki yao ya kupata habari. Kati ya humusi moja hadi mbili ya watoto na vijana wanaweza kuchukuliwa kuwa 'watafuta-habari', kwa kuwa wanafanya utafutaji wa habari mbalimbali mtandaoni kila wiki - kujifunza kitu kipya, kujua kuhusu kazi au fursa za masomo, kutafuta habari, kusaka taarifa za afya au za matukio karibu nao.

Watoto wengi na vijana wa umri wote hutumia mtandao kwa kazi za nyumbani, au hata kujifunza mambo waliokosa kwa kutohudhuria masomo.


“Walituomba tutafute majina ya mawaziri nchini Ghana, kutafuta nchi na sarafu zao. Unaweza kupata habari kuhusu nchi nyingine.” Msichana, mwenye umri wa miaka 12-14, Ghana


"Kwenye Intaneti, tunaweza kutafuta vitu vyote tunavyohitaji shuleni, na hatuwezi kupata katika vitabu." Msichana, mwenye umri wa miaka 9, Serbia

"Nilifeli hisabati, kwa hiyo nilitazama video kadhaa ambazo zilieleza nilichopaswa kujifunza." Mvulana, mwenye umri wa miaka 15-17, Argentina

"Ikiwa huendi shuleni, unaweza kuzungumza na rafiki yako na kujua ulichokosa na mengine kama hayo. Kwa hivyo, ni muhimu, kuwa na WhatsApp ya rafiki yako." Msichana, mwenye umri wa miaka 16-17, Afrika Kusini

**Kielelezo cha 4: Watoto (%) ambao hufanya shughuli tatu au zaidi za kutafuta habari angalau kila wiki, kulingana na jinsia na umri.** [21]




| | |
|---|---|
| Swali C4: Je, umefanya shughuli za kutafuta habari mara ngapi mtandaoni katika mwezi uliopita? Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti | Swali C4: Je, umefanya shughuli za kutafuta habari mara ngapi mtandaoni katika mwezi uliopita? Msingi: Watoto wote wanaotumia Intaneti |

Kielelezo cha 4 kinaonyesha chati mbili za upau zinazoonyesha majibu ya uchunguzi wa matumizi ya Intaneti miongoni mwa watoto kwa shughuli za kutafuta taarifa mtandaoni katika mwezi uliopita: Chati moja inaonyesha mgawanyo wa matumizi kati ya wasichana na wavulana, na matumizi sawa kwa wavulana na wasichana. Chati nyingine inaonyesha mgawanyo kulingana na umri. Hii inaonyesha kuwa katika nchi zote isipokuwa moja ya nchi zilizofanyiwa utafiti, kundi la watoto wa miaka 9-11 walitumia Intaneti kwa shughuli za ubunifu mtandaoni mara chache kuliko vikundi vingine viwili vya umri (watoto wa miaka 12-14 na wenye umri wa miaka 15-17).) na kwa nchi zote zilizochunguzwa, kikundi cha watoto wa miaka 15-17 kiliitumia zaidi kutafuta habari.

Kumbuka: Watoto na vijana waliulizwa ni mara ngapi walifanya shughuli zifuatazo za kutafuta habari katika mwezi uliopita: walijifunza kitu kipya kwa kutafuta mtandaoni; walitafuta habari kuhusu nafasi za kazi au masomo; walitumia mtandao kwa kazi za shule; walitafuta rasilimali au matukio karibu nao; walitafuta habari mtandaoni; walijitafutia taarifa za afya wao wenyewe au mtu wanayemjua. Argentina imeachwa kwa sababu ya kukosa data.

Asili: UNICEF

[21] Mchoro huu ulitolewa kwenye: UNICEF (2019). *Growing up in a connected world*. UNICEF Office of Research - Innocenti, Florence, https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20Summary%20Report.pdf.

- Matumizi ya teknolojia ya Intaneti kwa watoto na vijana yameongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni na yameambatana na wasiwasi unaoongezeka kuhusu masuala ya usalama mtandaoni. Kihistoria, kumekuwa na hofu ya mara kwa mara ya kimaadili kuhusu hatari inayoweza kutokea ya teknolojia ya mawasiliano, na hii imekuwa hasa kwa Watoto wa kike. Hata hivyo, inasemekana kwamba hatari hizo zinapochunguzwa, inaonekana kwamba mara nyingi sana si teknolojia ndiyo chanzo chake bali ni ongezeko la shughuli za watoto na vijana wanaotumia teknolojia hiyo, zaidi wasiwasi kuhusu kupoteza udhibiti wa wazazi. Waelimishaji wamechukuliwa kuwa na jukumu muhimu katika kukuza na kuhakikisha usalama wa Mtandao. Wazazi kote ulimwenguni wanaonekana kuamini kuwa shule zinapaswa kuwa na jukumu kuu katika kuelimisha watoto na vijana katika matumizi salama ya teknolojia, lakini pia ni wazi kutokana na utafiti kwamba chanzo kikuu cha habari juu ya maswala ya mtandaoni kwa watoto na vijana ni kutoka shuleni na kutoka kwa wazazi.[66]

[66] Ofcom (2020), Children and Parents: Media Use and Attitudes Report 2019, *https://www.ofcom.org.uk/__data/assets/pdf_file/0024/190518/children-media-use-attitudes-2019-chart-pack.pdf*.

- Mwongozo zaidi kuhusu umilisi unaopaswa kujumuishwa katika aina hii ya elimu ulitambuliwa kama sehemu ya mradi wa elimu ya uraia wa Dijitali wa Baraza la Ulaya. [67]

**Kielelezo cha 8: Watoto wakisema iwapo wamepewa taarifa au ushauri wowote kuhusu jinsi ya kutumia Intaneti kwa usalama, miongoni mwa wale wanaotumia mtandao nyumbani (2012) au kwingineko (2017, 2018, 2019), kulingana na umri. [68]**

| Taarifa zozote zilizopokelewa | Kutoka kwa mwalimu | Kutoka kwa mzazi | Kutoka kwa marafiki | Kutoka kwa jamaa mmoja wa familia | Kutoka kwa polisi wanaokuja shuleni** | Kutoka kwa tovuti | Kutoka kwa TV/vipindi vya redio |
|---|---|---|---|---|---|---|---|




Kielelezo cha 8 Watoto wakisema wamepewa maelezo au ushauri kuhusu jinsi ya kutumia Intaneti kwa usalama, miongoni mwa wale wanaotumia mtandao nyumbani (2012) au kwingineko (2017, 2018, 2019), kulingana na umri (8 hadi 11 na 12 hadi 15) inaonyesha mfululizo wa miaka katika chati za upau kulingana na umri ikionyesha iwapo taarifa yoyote imepokelewa au la, na kutoka kwa vyanzo saba: kutoka kwa mwalimu, mzazi, kutoka kwa marafiki, kutoka kwa jamaa mwingine wa familia, kutoka kwa polisi wanaokuja shuleni, kutoka kwa tovuti, kutoka kwa TV. / vipindi vya redio. Kwa vyanzo vingi, kuna ongezeko la kasi la idadi ya Watoto hao katika 2012, 2017, 2018 na 2019.

Asili: Ofcom

[67] Council of Europe (2018), *Guidelines to Respect, Protect and Fulfil the Rights of the Child in the Digital Environment, Recommendation CM/Rec (2018)7 of the Committee of Ministers, Building a Europe for and with Children*, *https://rm.coe.int/guidelines-to-respect-protect-and-fulfil-the-rights-of-the-child-in-th/16808d881a* .

[68] Ofcom (2020), *Children and Parents: Media Use and Attitudes Report 2019*, *https://www.ofcom.org.uk/__data/assets/pdf_file/0024/190518/children-media-use-attitudes-2019-chart-pack.pdf*.

• Mbinu za awali za usalama mtandaoni zililenga zaidi suluhu za kiteknolojia, kama vile matumizi ya programu za kuchuja, lakini katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko la mabadiliko ya teknolojia ya habari na kwa sababu hiyo, kompyuta nyingi za mezani si mahali pekee pa kufikia intaneti. Kuongezeka kwa idadi ya simu za mkononi, kompyuta za mkononi, visaidizi vya kibinafsi vya kidijitali na vifaa vya michezo ya kubahatisha vinatoa miunganisho ya mitandao-kasi na watoto na vijana wanaweza kupata Intaneti wakiwa shuleni, nyumbani, kwenye maktaba, kwenye migahawa ya Internet, hoteli za vyakula vya haraka, katika vilabu vya vijana au hata kwenye vyombo vya usafiri wa umma. Shule hutoa fursa ya kufanya kazi kwenye mtandao, kwa ushirikiano katika eneo la mtandao uliofungiwa au kuzungukwa tu na Watoto na vijana. Hatua za awali za dhahiri ni pamoja na kuweka usalama madhubuti katika mtandao. Watoto na vijana wanaweza kuwa na vifaa vya kibinafsi ambavyo havina ulinzi wa mtandao na hii ndiyo sababu elimu, majadiliano na mazungumzo ni muhimu.

• Sera za usalama mtandaoni zinahitaji kubuniwa na kutekelezwa kwa kuhusisha makundi mbalimbali na wadau tofautitofauti. Wadau hao ni pamoja na:

- wakuu wa shule;
- viongozi;
- usimamizi mwandamizi;
- walimu wa darasa;
- wafanyakazi wadogo;
- wazazi au walezi;
- wafanyakazi wa serikali za mitaa;
- inapowezekana, watoa huduma za Intaneti na mitandao-kasi kwenye mashule.

Kwa vile makundi haya yote yana maarifa ambayo yanaweza kusaidia kuweka sera za shule, ni muhimu kwamba yote yashauriwe. Hata hivyo, kuwa na sera tu haitoshi na, kila mtu anayehusika na watoto na vijana wanapaswa kufanya mazoea madhubuti ambayo yatasaidia wafanyikazi kutambua na kufikia tabia salama. Kwa kuhusisha vikundi hivi vyote tangu mwanzo, kila mtu anapaswa kuhisi umuhimu wa sera kama hizo na vile vile jukumu lao la kibinafsi la kuzifanya kuwa za kweli.

Kuunda mazingira salama ya kujifunza TEHAMA kuna mambo kadhaa muhimu, ambayo ni pamoja na yafuatayo:

- miundombinu ya uhamasishaji wa tovuti nzima;
- majukumu, sera na taratibu;
- safu madhubuti ya zana za kiteknolojia;
- elimu ya kina ya usalama wa kielektroniki;
- mpango kwa kila mtu katika taasisi;
- mchakato wa ukaguzi ambao hufuatilia kila mara ufanisi wa mazingira ya kujifunza ya TEHAMA.

Haya yote yanapaswa kufumbatwa katika sera zilizopo za usalama wa mtoto ndani ya shule, badala ya kuonekana kama kitu kinachosimamiwa na timu ya TEHAMA pekee. Haileti mantiki kufikiri kuhusu uchokozi kwenye Mtandao au kupitia simu ya mkononi kama kitu tofauti na uchokozi katika ulimwengu wa nje ya mtandao. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa teknolojia pia haiwezi kuwa sehemu muhimu ya suluhisho kupitia:

- kuzuia na kudhibiti virusi;
- mifumo ya ufuatiliaji ili kujua nani alipakua nini, kilipakuliwa lini, na kompyuta gani ilitumika;
- kuchuja na kudhibiti maudhui ili kupunguza yasiyofaa kupitia intaneti ya shule.

Matatizo yanayotokea kuhusiana na teknolojia mpya hayatumiki kwa watoto na vijana wote, na matatizo yanapotokea, yanategemea umri wa watoto na vijana wanaotumia teknolojia hizi. Mwishoni mwa 2008, Kikosi Kazi cha Kiufundi cha Usalama wa Mtandao nchini Marekani kilitoa ripoti juu ya kuimarisha usalama wa watoto na teknolojia za mtandaoni ambapo ilitoa tathmini muhimu ya kazi ya utafiti asilia, ilichapisha utafiti wa kushughulikia ushawishi wa kingono mtandaoni, unyanyasaji na uchokozi mtandaoni, na kufichuliwa kwa maudhui hatarishi. [69] Ndani ya ripoti hii ilibainishwa kuwa, "Kuna wasiwasi kwamba vyombo vya habari vya kawaida vinaongeza hofu hizi, na kuzifanya kuwa zisizolingana na hatari zinazokabili vijana." Ni zaidi ya miaka kumi baadaye na hii bado ndiyo hali ya wazazi na waelimishaji wakiangaziwa na vichwa vya habari dumavu ambavyo vinaweza kuwahimiza watu wazima kudhibiti ufikiaji wa huduma za mtandao badala ya kuelimisha na kuwawezesha watoto kuzitumia kwa usalama.

Hii inaibua hofu kwamba hatari zinazojulikana zitabaki zimefichwa na kupunguza uwezekano kwamba jamii itashughulikia sababu zinazochangia uwepo wazo, ambapo hali hii inaweza kuleta madhara bila kukusudia. Uangaziaji wa vyombo vya habari kuhusu uhalifu wa mtandaoni dhidi ya watoto na vijana mara nyingi huonekana kuakisi misimamo iliyogawanyika ya wataalamu na wasomi wanaofanya kazi katika eneo hilo, huku mpaka ukionekana kati ya wale wanaohisi kuwa kuna hatari ya upotoshaji dhidi ya watoto na vijana, na wale ambao inaonekana kwamba tishio limepuuzwa.

Hata hivyo, kuna wasiwasi kwamba teknolojia ya mtandao inaweza kuwaacha baadhi ya watoto na vijana katika mazingira magumu na kwamba waelimishaji, pamoja na wazazi na walezi, wana wajibu kuhusiana na hili. Njia tofauti ambazo watoto na vijana wanaweza kudhulumiwa mtandaoni ni pamoja na:

- kushawishi watoto kwa ngono;
- hatari ya kutangamana na nyenzo zenye mushkili au zisizo halali;

[69] ISTTF (2008), *Enhancing Child Safety and Online Technologies: Final Report of the Internet Safety Technical Task Force to the Multi-State Working Group on Social Networking of State Attorneys General of the United States*, *https://cyber.harvard.edu/sites/cyber.law.harvard.edu/files/IS TTF_Final_Report.pdf*.

- hatari ya kukumbana na vyombo vinavyoweza kukuza mwenendo mbaya kwa upande wa vijana;
- unyanyasaji mtandaoni.

Njia muhimu ya kuainisha hatari za mtandaoni kwa watoto iliwasilishwa katika Kielelezo cha 7.

### Mazingira ya elimu isiyo rasmi

Kando ya shule na nyumbani, watoto wanaweza kufikia Mtandao na kutumia huduma zake katika mazingira yasiyokuwa hayo k.m. vilabu vya vijana au vikundi vya kanisa. Kuingiliana kwa maisha ya mtandaoni na nje ya mtandao kwa watoto na vijana kunamaanisha kwamba wale wanaofanya kazi na watoto katika mipangilio kama hii wanaweza kuwa na ushawishi kwa watoto walio kwenye mazingira ya kidijitali na usalama wao mtandaoni, hata kama hilo sio lengo lao kuu. Kwa hivyo, wale wote wanaofanya kazi katika mazingira yasiyo rasmi wanapaswa kuwa na uelewa fulani wa hatari na fursa na waweze kusaidia watoto ipasavyo au kupata usaidizi na mafunzo wanayohitaji.

Mambo muhimu ya kuzingatia na kanuni za miongozo ya waelimishaji pia hutumika katika mazingira kama haya, hata hivyo, kunaweza kuwa na tofauti za kimazingira au mambo ya ziada ya kuzingatia.

### Kusimamia vifaa, uchujaji na mawasiliano

Wafanyakazi wadogo, wanaojitolea na watoto wanaweza kuwa na uwezo mkubwa wa kufikia huduma kupitia vifaa vyao wenyewe katika mipangilio isiyo rasmi au mifumo ya kudhibiti vifaa, na huenda maudhui yaliyochujwa yasipatikane au yasiwe na nguvu kuliko shuleni. Kwa hivyo, kuhakikisha kwamba wahudumu na watoto wanaelewa jinsi ya kulinda na kudhibiti kifaa chao wenyewe panaweza kuwa na haja ya kuwaangazia zaidi katika mipangilio isiyo rasmi. Sawa na chaguzi zisizo za kisasa zaidi za kuchuja zinazopatikana, waelimishaji na watoto hawapaswi kuzitegemea sana kwa ulinzi.

Mipangilio isiyo rasmi bado inapaswa kuwa na sera na miongozo thabiti yenye kupiga jeki ulinzi wa mtoto - hata hivyo katika baadhi ya mipangilio waelimishaji au msaragambo wanaweza kukosa ufikiaji wa kifaa cha shirika au akaunti ya barua pepe katika mipangilio hii. Kwa hivyo, uzingatiaji wa ziada utahitajika kwa matumizi ya vifaa vya kibinafsi na ikiwa/jinsi hii inafuatiliwa/inasimamiwa kwa usalama katika sera na utendaji.

Vile vile, bila kufikia ‘elimu ya’ teknolojia, vifaa na usaidizi wa 'kielimu' panaweza kuwa uwezekano mkubwa kwamba mitandao ya kijamii na huduma za ujumbe zitatumiwa mara kwa mara katika mazingira yasiyo rasmi kuliko shuleni. Kwa hivyo, mazingatio zaidi yanaweza kuhitajika katika sera ya shirika, mazoezi na mafunzo ili kutambua kama/jinsi hizi zinatumika na kusimamiwa kwa usalama.

### Mafunzo na msaada

Waelimishaji na watu wa kujitolea wanaofanya kazi katika mazingira yasiyo rasmi wanaweza kuwa na nafasi ndogo ya kujihusisha na mafunzo, kuboresha ujuzi wao au kupata usaidizi mbalimbali ambao unaweza kupatikana kwa waelimishaji katika mazingira rasmi. Yapaswa kuzingatiwa jinsi mashirika yasiyo rasmi hupata, kutoa na kufadhili mafunzo na usaidizi wa aina hii.

Jedwali la 2 linabainisha baadhi ya vipengee muhimu ambavyo waelimishaji wanapaswa kuzingatia.

## 10. Miongozo kwa waelimishaji

Inakubalika kuwa walimu/waelimishaji binafsi hawatakuwa na udhibiti wa baadhi ya vipengee vya kuzingatiwa katika Jedwali 2 hapa chini, kama vile kuchuja na ufuatiliaji. Inatarajiwa kwamba hatua hizi zitachukuliwa na shule au mazingira ya elimu.

**Jedwali 2: Mambo muhimu ya kuzingatia kwa waelimishaji**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **#** | **Mambo muhimu ya kuzingatia** | **Maelezo** |
| Usalama na ulinzi wa vifaa | 1 | Hakikisha kuwa vifaa vyote viko salama na nenosiri linalindwa. | Walimu wako katika hatari kama mtu mwingine yeyote kwa mashambulizi ya mtandaoni, programu hasidi, virusi na udukuzi. Ni muhimu kwamba walimu wahakikishe kuwa kifaa chochote wanachotumia kinalindwa ipasavyo (na manenosiri thabiti) na kimefungwa wakati hakitumiki. (k.m. ikiwa mwalimu anahitaji kuondoka darasani, basi kifaa chochote anachotumia kifungwe au mwalimu aondoke/kutoka nje). |
| | 2 | Sakinisha programu ya kuzuia virusi na ngome ya firewalls | Hakikisha kuwa vifaa vyote vina ngome ya firewall na programu ya kuzuia virusi iliyosakinishwa na kwamba hii inasasishwa. |
| Sera | 3 | Shule zote zinapaswa kuwa na sera ambayo inasimamia mahali na jinsi gani teknolojia inaweza kutumika shuleni na wadau mbalimbali na jinsi shughuli za ulinzi wa watoto zinavyoendeshwa - ikiwa ni pamoja na mtandaoni. | Walimu wanapaswa kuhakikisha kuwa wanafuata sera kuhusu matumizi ya teknolojia ya simu na vifaa vingine vya kielektroniki. Ni muhimu kwamba walimu waige tabia sahihi wanapotumia vifaa. Shule zinafaa kubainisha ni wapi na lini vsimu za mkononi zinaweza kutumika. |
| | 4 | Picha za wanafunzi. | Shule zinapaswa kuwa na sera inayofafanua ikiwa picha za wanafunzi zinaweza kuchukuliwa. Je, wafanyakazi wanaweza kupiga picha kwa madhumuni ya elimu? Je, ruhusa husika imetolewa na wazazi/walezi/wanafunzi wenyewe? Kimsingi sera inapaswa kueleza kuwa vifaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | vya kibinafsi havifai kutumika kwa madhumuni haya ili kuwalinda wanafunzi na wafanyakazi. |
| Kuchuja na ufuatiliaji | 5 | Hakikisha kwamba taarifa za Intaneti zinazotolewa na shule zinachujwa na kufuatiliwa. | Wanafunzi hawapaswi kupata maudhui yenye madhara au yasiyofaa kutoka kwa mifumo ya TEHAMA ya shule. Hakuna mfumo wa kuchuja unaoweza kuwa na ufanisi wa asilimia 100 na ni muhimu kupiga jeki suluhu hizi za kiufundi kwa ufundishaji na ujifunzaji mzuri pamoja na usimamizi mzuri. Kwa uchache uchujaji unapaswa kuzuia ufikiaji wa maudhui haramu pamoja na maudhui yanayochukuliwa kuwa yasiyofaa au yenye madhara. Kwa mfano, aina zifuatazo za maudhui hatari zinapaswa kuzingatiwa:<br>• Ubaguzi<br>• Matamshi ya chuki<br>• Matumizi mabaya ya dawa au dawa za kulevya<br>• Itikadi mkali<br>• Ponografia<br>• Uharamia na wizi wa hakimiliki<br>• Kujidhuru au kujiua<br>• Ghasia za kiwango kikubwa |
| Hadhi ya Mtandaoni/alama za kidijitali | 6 | Kufahamu umuhimu wa alama za kidijitali na hadhi ya mtandaoni. | Walimu wanapaswa kufahamu kwamba wanachosema na kufanya mtandaoni kinaweza kuathiri hadhi yao na pia sifa ya shule/chuo.<br>Walimu wanapaswa kutenda kwa njia ya kitaaluma kila wakati mtandaoni. Watoto pia wanapaswa kufundishwa kuhusu umuhimu wa sifa mtandaoni na jinsi ya kudumisha hili kwa ufanisi. |
| Jinsi ya kuwasiliana kwa usalama kitaaluma | 7 | Kutambua umuhimu wa mawasiliano ya kitaalamu mtandaoni | Daima kuwe na mpaka wazi kati ya maisha ya kibinafsi ya mwalimu na maisha yake ya kitaaluma - hii inajumuisha shughuli za mtandaoni. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | na wanafunzi, wazazi na wadau wengine. | Barua pepe ya shule inapaswa kutumika kila wakati kwa mawasiliano yoyote kati ya wafanyikazi na wanafunzi au wazazi. Shule zinaweza kutaka kuhakikisha sera za mawasiliano au kanuni za maadili zinakataza mawasiliano ya ana kwa ana na mawasiliano yoyote bila malengo ya kielimu au kwenye mifumo isiyo ya shule.<br>Vyombo vya kibinafsi visitumike kuwasiliana na wanafunzi au wazazi/walezi.<br>Mawasiliano ya ana kwa ana ya kidijitali yanapaswa kuepukwa.<br>Ikiwa mkutano wa video au mafunzo ya mbali yanafanyika, shule zinapaswa kuwa wazi kuhusu matarajio ya wafanyakazi na wanafunzi. (k.m. kufikiria mahali ambapo masomo/mawasiliano ya kidijitali yanafanyika yaani si katika chumba cha kulala - zingatia wengine ambao wanaweza kuwa karibu nawe nyumbani/darasani.) |
| Mwenendo wa mwanafunzi na hali hatarishi mtandaoni na athari yake kwa ulinzi na ustawi | 8 | Kuelewa hatari na manufaa ambayo wanafunzi wanaweza kukabiliwa nayo wanapoingia mtandaoni | Walimu wanahitaji kuelewa kile watoto na vijana wanafanya wanapotumia mtandao na hatari na manufaa wanayoweza kukumbana nayo. |

## 11. Hitimisho

Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) imebadilisha maisha ya kisasa. Imetusahilishia mawasiliano, ufikiaji usio na mipaka na ulio karibu wa habari na huduma mbalimbali za ubunifu. Wakati huo huo, pia imeunda majukwaa mapya ya dhuluma na unyanyasaji. Bila ya ulinzi ufaao, watoto na vijana - miongoni mwa watumiaji wakubwa zaidi wa Mtandao - wako katika hatari ya kushawishiwa kingono, unyanyasaji, na hatari ya kukumbwa na nyenzo zenye vurugu, ngono na nyingine zisizohitajika.

Bila njia sahihi za kuunda mazingira salama ya mtandao, watoto na vijana watabaki kuwa hatarini. Ingawa kuna ongezeko la ufahamu wa hatari zinazohusiana na matumizi yasiyo salama ya TEHAMA, bado kuna kiasi kikubwa cha kazi ya kufanya. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba wazazi na waelimishaji wajadili na kuamua na watoto na vijana kuhusu mambo yanayofaa na salama kwa matumizi yao, pamoja na jinsi ya kuishi vizuri wakiendelea kutumia TEHAMA.

Katika kufanya kazi pamoja, wazazi, waelimishaji, watoto na vijana wanaweza kupata manufaa ya TEHAMA, wakati huo huo wakipunguza hatari zinazoweza kutokea kwa watoto na vijana.

## Istilahi

Ufafanuzi ulio hapa chini umetolewa hasa kutokana na istilahi zilizopo kama zilivyofafanuliwa katika Mkataba wa Haki za Mtoto, 1989, na vile vile kikundi kazi cha mashirika kuhusu unyanyasaji kingono kwa watoto katika Miongozo ya Istilahi kuhusu Ulinzi wa Watoto dhidi ya Unyanyasaji wa Kimapenzi na Dhuluma ya Ngono, 2016[70] (Mwongozo wa Luxembourg), na Mkataba wa Baraza la Ulaya: Ulinzi wa Watoto dhidi ya Unyanyasaji wa Kimapenzi na Unyanyasaji wa Ngono, 2012[71] na vile vile na Ripoti ya Global Kids Online, 2019. [72]

***Kijana aliyebaleghe***

Vijana waliobaleghe ni watu wenye umri wa miaka 10-19. Ni muhimu kutambua kwamba neno vijana *baleghe* si istilahi inayoonyesha ulazima katika sheria ya kimataifa, na wale walio chini ya umri wa miaka 18 wanachukuliwa kuwa watoto, huku wenye miaka 19 wanachukuliwa kuwa watu wazima, isipokuwa ikiwa wengi watafikia umri huo mapema chini ya sheria ya kitaifa. [73]

[70] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf* .
[71] Council of Europe (2012), *Protection of Children against Sexual Exploitation and Sexual Abuse: Council of Europe Convention*, *https://www.coe.int/t/dg3/children/1in5/Source/Lanzarote%20Convention_EN.pdf* .
[72] Globalkidsonline.net (2019), *Done Right, Internet Use Can Increase Learning and Skills,* *http://globalkidsonline.net/synthesis-report-2019/* .
[73] UNICEF and ITU (2015), *Guidelines for Industry on Child Online Protection*, *https://www.itu.int/en/cop/Documents/bD_Broch_INDUSTRY_0909.pdf* .

### *Akili Bandia (AI)*

Kwa maana pana, neno hili linarejelea waziwazi mifumo ambayo ni bunilizi za kisayansi tu (yaani AI "thabiti" zenye mfumo unaojitambua) na mifumo ambayo tayari inafanya kazi na yenye uwezo wa kufanya shughuli changamano sana (kutambua uso au sauti; kuendesha gari - mifumo hii inaelezwa kama AI "dhaifu" au "wastani").[74]

### *Mifumo ya AI*

Mfumo wa AI ni mfumo unaotegemea mashine na ambao unaweza, kwa malengo fulani yaliyobainishwa na binadamu, kufanya ubashiri, mapendekezo, au maamuzi yanayoathiri mazingira halisi au ya mtandaoni, na umeundwa kufanya kazi kwa viwango tofauti vya uhuru. [75]

### *Alexa*

**Amazon Alexa,** inayojulikana kama **Alexa**, ni kisaidizi cha kawaida cha AI kilichotengenezwa na Amazon. Kina uwezo wa kuzungumza, kucheza muziki, kutengeneza orodha ya mambo ya kufanya, kuweka kengele, kutiririsha podikasti, kusoma vitabu kwa sauti na kutoa taarifa za hali ya hewa, trafiki, spoti na taarifa za punde, kama vile habari. Alexa pia inaweza kudhibiti vifaa kadhaa mahiri ikijiendesha yenyewe kiotomatiki nyumbani. Watumiaji wanaweza kupanua uwezo wa Alexa kwa kusakinisha "ujuzi" (utendaji wa ziada uliotengenezwa na waundaji wengine, katika mipangilio mingine inajulikana zaidi kama programu za hali ya hewa na vipengee vya sauti). [76]

### *Maslahi bora ya mtoto*

Inaelezea vipengele vyote muhimu vinavyohitajika kufanya maamuzi katika hali maalum kwa mtoto maalum au kikundi cha watoto. [77]

### *Mtoto*

Kwa mujibu wa kifungu cha 1 cha Mkataba wa Haki za Mtoto, mtoto ni mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka 18, isipokuwa kwa makubaliano ya wengi kuhusu umri wa mapema chini ya sharia za taifa. [78]

---

[74] Council of Europe (2020), *What's AI? https://www.coe.int/en/web/artificial-intelligence/what-is-ai .*

[75] OECD (2019), *Recommendation of the Council on Artificial Intelligence*, *https://webcache.googleusercontent.com/search?q=cache:hTtMv9k1ak8J:https://legalinstruments.oecd.org/api/print%3Fids%3D648%26lang%3Den+&cd=3&hl=en&ct=clnk&gl=ch&client=safari*.

[76] Amazon (2019), *Alexa Skills Kit Official Site: Build Skills for Voice*, *https://developer.amazon.com/en-US/alexa/alexa-skills-kit .*

[77] OHCHR (1990) , *Convention on the Rights of the Child, https://www.ohchr.org/en/professionalinterest/pages/crc.aspx*.

[78] UNICEF and ITU (2015), *Guidelines for Industry on Child Online Protection*, *https://www.itu.int/en/cop/Documents/bD_Broch_INDUSTRY_0909.pdf*

***Dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto (CSEA)***

Inafafanua aina zote za dhuluma za kingono na unyanyasaji wa kijinsia (CRC, 1989, kifungu cha 34), k.m. "(a) kushawishi au kushurutishwa kwa mtoto kujihusisha na shughuli zozote za ngono zisizo halali; (b) Kuwadhulumu watoto katika ukahaba au matendo mengine ya ngono yasiyo halali; (c) Kuwatumia watoto kingono kwa kutumia nyenzo za ponografia" na vilevile "kufanya ngono ambako kwa kawaida kutumia nguvu dhidi ya mwathiriwa bila ruhusa yake." [79] Unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa watoto unazidi kufanyika kupitia Mtandao, au kwa uhusiano fulani na mazingira ya mtandaoni. [80]

***Nyenzo za kwanyanyasa kingono watoto (dhuluma na) (CSAM)***

Mageuzi ya haraka ya TEHAMA yameunda aina mpya za dhuluma na unyanyasaji wa kingono kwa watoto mtandaoni, ambao unaweza kufanyika kiuhalisia na si lazima uhusishe kukutana ana kwa ana na mtoto. [81] Ingawa mamlaka nyingi bado zinaweka lebo ya picha na video za unyanyasaji wa kingono kwa watoto 'ponografia ya watoto' au 'picha zisizofaa za watoto', miongozo hii itarejelea wahusika kijumla kama nyenzo za unyanyasaji wa kingono kwa watoto (kuanzia sasa, CSAM). Hii ni kulingana na Miongozo ya Kamisheni ya Broadband na vuguvugu la WePROTECT Global Alliance Model National Response.[82]. Neno hili linafafanua maudhui kwa usahihi zaidi. Kwamba ponografia ni tasnia halali iliyojengeka kibiashara, na kama miongozo ya Luxemburg inavyosema, matumizi ya neno hili:

"huenda (bila kukusudia au kwa kukusudia) ikachangia kupunguza nguvu ya, kudharau, au hata kuhalalisha kile ambacho hasa ni unyanyasaji wa kingono na/au dhuluma za kingono kwa watoto [...] neno 'ponografia ya watoto' lina hatari kuashiria kwamba vitendo hivyo vinatekelezwa kwa idhini ya mtoto, na kuwakilisha nyenzo halali za ngono". [83]

Neno CSAM linarejelea nyenzo zinazowakilisha vitendo vya unyanyasaji wa kingono na/au dhuluma dhidi ya mtoto. Hii inahusisha, lakini haijikiti tu kwa, vifaa vinavyotumiwa kurekodi

---

[79] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf* .

[80] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf* .

[81] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf* .;" UNICEF and Global Kids Online (2019), *Global Kids Online Comparative Report*, *https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20LAYOUT%20MAIN%20REPORT.pdf*.

[82] WePROTECT Global Alliance (2016), *Preventing and Tackling Child Sexual Exploitation and Abuse (CSEA): A Model National Response*.,
*https://static1.squarespace.com/static/5630f48de4b00a75476ecf0a/t/582ba50bc534a51764e8a4ec/1479255310190/WePROTECT+Global+Alliance+Model+National+Response+Guidance.pdf* ; Broadband Commission (2019), *Child Online Safety: Minimizing the Risk of Violence, Abuse and Exploitation* Online, *https://broadbandcommission.org/Documents/working-groups/ChildOnlineSafety_Report.pdf* .

[83] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf*

unyanyasaji wa kingono wa watu wazima dhidi ya watoto; picha za watoto zenye kuonyesha ngono yao; sehemu za siri za watoto wakati picha hizo zinatolewa au kutumika kwa madhumuni ya ngono.

***Watoto na vijana***

Inaelezea watu wote walio chini ya umri wa miaka 18 ambapo watoto, wanaojulikana kama watoto wadogo kwa mujibu wa miongozo inayorejelea watu wote walio chini ya umri wa miaka 15, na vijana wanajumuisha kikundi cha watu wenye umri wa miaka 15 hadi 18.

***Vidude vya watoto vya kuchezea vilivyounganishwa***

Hivi ni vidude vya kuchezea vilivyounganishwa kwenye Mtandao kwa kutumia teknolojia kama vile Wi-Fi na Bluetooth, na kwa kawaida hufanya kazi pamoja na programu shirikishi ili kuwezesha uchezaji unaoamiliana na watoto. Kulingana na Utafiti wa Juniper, soko la vidude vya kuchezea vilivyounganishwa lilifikia dola bilioni 2.8 katika 2015 na inatabiriwa kuongezeka hadi dola bilioni 11 ifikapo 2020. Vidude hivi vya kuchezea hukusanya na kuhifadhi taarifa za kibinafsi kutoka kwa watoto ikiwa ni pamoja na majina, eneo, anwani, picha, sauti na video zilizorekodiwa. [84]

***Unyanyasaji mtandaoni, pia unajulikana kama Uchokozi Mtandaoni***

Unyanyasaji mtandaoni hufafanua kitendo cha uchokozi cha kukusudia kinachofanywa mara kwa mara na kikundi au mtu binafsi kwa kutumia teknolojia ya kidijitali na kumlenga mtu ambaye hawezi kujitetea kwa urahisi.[85] Kwa kawaida huhusisha "kutumia teknolojia ya kidijitali na Mtandao kuchapisha habari zenye kumuumiza mtu fulani, kusambaza habari za faragha, picha au video kimakusudi kwa njia ya kuumiza, kutuma ujumbe wa vitisho au matusi (kupitia barua pepe, ujumbe wa papo hapo, chati, jumbe fupi), kueneza uvumi na matusi. habari za uwongo kuhusu mwathiriwa au kuwatenga kwa makusudi kutoka kwa mawasiliano ya mtandaoni". [86] Inaweza kuhusisha uchapishaji wa moja kwa moja wa mawasiliano (kama vile chati au ujumbe mfupi), hadharani (kama vile kuchapisha ujumbe wa unyanyasaji kupitia barua pepe) au mawasiliano ya umma (kama vile kuunda tovuti inayolenga kumdhihaki mwathiriwa).

---

[84] Jeremy Greenberg (2017), *Dangerous Games: Connected Toys, COPPA, and Bad Security*, *https://georgetownlawtechreview.org/dangerous-games-connected-toys-coppa-and-bad-security/GLTR-12-2017/*.

[85] Anna Costanza Baldry, Anna Sorrentino, and David P. Farrington (2019), *Cyberbullying and Cybervictimization versus Parental Supervision, Monitoring and Control of Adolescents' Online Activities*, *https://doi.org/10.1016/j.childyouth.2018.11.0058*.

[86] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf* .;"UNICEF and Global Kids Online (2019), *Global Kids Online Comparative Report*, *https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20LAYOUT%20MAIN%20REPORT.pdf*

***Chuki za mitandaoni, ubaguzi, na itikadi kali za vurugu***

"Chuki za mtandaoni, ubaguzi na itikadi kali za vurugu ni aina tofauti ya unyanyasaji wa mtandaoni kwa kuwa unalenga utambulisho wa pamoja, badala ya watu binafsi […] mara nyingi kuhusiana na rangi, mwelekeo wa kijinsia, dini, utaifa au hali ya uhamiaji, uana/jinsia na siasa"[87].

***Uraia kidijitali***

Uraia kidijitali unarejelea uwezo wa kujihusisha vyema, kwa umakinifu na kwa umahiri katika mazingira ya kidijitali, kwa kutumia ujuzi wa mawasiliano na ubunaji ulio madhubuti, kushiriki katika masuala ya kijamii yanayoheshimu haki za binadamu na utu kwa kutumia teknolojia kwa njia bora. [88]

***Ufahamu wa kidijitali***

Ufahamu wa kidijitali unamaanisha ujuzi anaohitaji mtu ili kuishi, kujifunza na kufanya kazi katika jamii ambapo mawasiliano na upataji wa taarifa huongezeka kupitia teknolojia za kidijitali kama vile majukwaa ya Intaneti, mitandao ya kijamii na vifaa vya mkononi. [89] Inajumuisha mawasiliano ya wazi, ujuzi wa kiufundi na fikra zenye tija.

***Ustahimilivu kidijitali***

Neno hili linaelezea uwezo wa mtoto wa kukabiliana kihisia na madhara anayokumbana nayo mtandaoni. Ustahimilivu wa kidijitali unahusisha hali ya kuwa na nyenzo za kihisia zinazohitajika ili kuelewa mtoto anapokuwa hatarini mtandaoni, kujua nini cha kufanya ili kutafuta usaidizi, kujifunza kutokana na uzoefu na kusaka suluhu mambo yanapoenda kombo. [90]

***Waelimishaji***

Mwelimishaji ni mtu ambaye anafanya kazi kwa utaratibu ili kuboresha uelewa wa mtu mwingine wa somo fulani. Jukumu la waelimishaji huhusisha walimu wa darasani na wale wasio rasmi zaidi ambao, kwa mfano, wanaotumia majukwaa na huduma za mitandao ya kijamii kutoa taarifa za usalama au kuendesha kozi za jumuiya au shule ili kuwawezesha watoto na vijana kukaa salama mtandaoni.

Kazi ya waelimishaji inatofautiana kulingana na mazingira wanayofanyia kazi na kundi la watoto na vijana wa umri fulani (au watu wazima) wanaopania kuelimisha.

---

[87] UNICEF and Global Kids Online (2019), *Global Kids Online Comparative Report*, *https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/GKO%20LAYOUT%20MAIN%20REPORT.pdf*.
[88] Council of Europe (date?), *Digital Citizenship and Digital Citizenship Education, https://www.coe.int/en/web/digital-citizenship-education/home.*
[89] Western Sydney University-Claire Urbach (date?), *What Is Digital Literacy? https://www.westernsydney.edu.au/studysmart/home/digital_literacy/what_is_digital_literacy*.
[90] Dr. Andrew K. Przybylski, et al. (2014), *A Shared Responsibility. Building Children's' Online Resilience Report*, *https://parentzone.org.uk/sites/default/files/Building%20Online%20Resilience%20Report.pdf*.

***Viongozi***

Hawa ni watu wote ambao wamewahi kushika nafasi ya usimamizi/mfumo wa utawala shule.

***Ushawishi wa ngono kwa watoto / Ushawishi wa ngono kwa watoto mtandaoni***

Hii ni kama ilivyofafanuliwa katika Miongozo ya Luxemburg, kwamba ni mchakato wa kuanzisha/kujenga uhusiano na mtoto aidha ana kwa ana au kwa kutumia Intaneti au teknolojia nyinginezo za kidijitali ili kuwezesha mawasiliano ya kingono mtandaoni na mtu huyo akimshawishi mtoto kuwa na uhusiano wa kimapenzi. [91] Mchakato unaokusudiwa kuwavuta watoto katika tabia ya ngono au mazungumzo na au bila wao kujua, au mchakato unaohusisha mawasiliano na utangamano kati ya mkosaji na mtoto ili kumfanya awe katika hatari zaidi ya unyanyasaji wa kingono. Kauli ushawishi wa ngono kwa mtoto haijafafanuliwa katika sheria za kimataifa; baadhi ya mamlaka, ikiwa ni pamoja na Kanada, hutumia neno 'kurubuni'.

***Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)***

Teknolojia ya habari na mawasiliano inaelezea teknolojia zote za habari zinazosisitiza kipengele cha mawasiliano. Hii ni pamoja na huduma na vifaa vyote vya kuunganisha Intaneti kama vile kompyuta, vipakatalishi, tableti, simu mahiri, vifaa vya michezo, televisheni na saa za mkononi.[92] Inajumuisha pia huduma kama vile za redio na vile vile mitandao-kasi, maunzi ya mtandao na mifumo ya setilaiti.

***Michezo ya mtandaoni***

'Michezo ya mtandaoni' inafafanuliwa kuwa aina yoyote ya mchezo wa dijitali wa kibiashara unaochezwa na mtu mmoja au wachezaji wengi kupitia kifaa chochote kilichounganishwa kwenye Intaneti, ikiwa ni pamoja na vifaa maalum, kompyuta za mezani, vipakatalishi, tableti na simu za mkononi.

'Mfumo wa michezo ya mtandaoni' unafafanuliwa kujumuisha kutazama wengine wakicheza michezo ya video kupitia e-sports, utiririshaji au majukwaa ya kusambaza video, ambayo kwa kawaida hutoa chaguo kwa watazamaji kutoa maoni au kutangamana na wachezaji na hadhira nyingineyo. [93]

***Zana za udhibiti za wazazi***

Programu ambayo inaruhusu watumiaji, kwa kawaida mzazi, kudhibiti baadhi au shughuli zote za kompyuta au kifaa kingine kinachoweza kuunganishwa kwenye Mtandao. Kwa kawaida,

---

[91] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf*

[92] UNICEF and ITU (2015), *Guidelines for Industry on Child Online Protection*, *https://www.itu.int/en/cop/Documents/bD_Broch_INDUSTRY_0909.pdf*.

[93] UNICEF (2019), *Child Rights and Online Gaming: Opportunities & Challenges for Children and the Industry*, *https://www.unicef-irc.org/files/upload/documents/UNICEF_CRBDigitalWorldSeriesOnline_Gaming.pdf*.

programu kama hizo zinaweza kupunguza ufikiaji wa aina fulani au aina za tovuti au huduma za mtandaoni. Baadhi pia hutoa wigo wa usimamizi wa wakati, yaani, kifaa kinaweza kuwekwa kuwa na ufikiaji wa Mtandao tu kati ya saa fulani. Matoleo ya juu zaidi yanaweza kurekodi maandishi yote yaliyotumwa au kupokewa kutoka kwa kifaa. Kwa kawaida programu zitalindwa kwa nenosiri. [94]

***Wazazi, watunzaji, walezi***

Tovuti kadhaa za Intaneti hurejelea wazazi kwa njia ya jumla (kama vile "ukurasa wa wazazi" na kurejelea "udhibiti wa wazazi") Kwa hivyo inaweza kuwa muhimu kufafanua watu ambao wanapaswa kuwawezesha watoto kuongeza fursa zinazopatikana mtandaoni, kuhakikisha kwamba watoto na vijana wanatumia tovuti za Intaneti kwa usalama na kwa uwajibikaji na kutoa kibali chao cha kuingia kwenye tovuti mahususi za mtandao. Katika hati hii, neno "wazazi" linamaanisha mtu yeyote (si waelimishaji) ambaye ana jukumu la kisheria kwa mtoto. Wajibu wa mzazi utatofautiana kati ya nchi na nchi kama ilivyo kwa haki za kisheria za wazazi.

***Taarifa za kibinafsi***

Neno hili linafafanua taarifa za kibinafsi zinazoweza kutambulika kuhusu mtu, zinazokusanywa mtandaoni. Hii ni pamoja na jina kamili, maelezo ya mawasiliano kama vile anwani za nyumbani na barua pepe, nambari za simu, alama za vidole au nyenzo za utambuaji wa uso, nambari za bima au sababu nyingine yoyote, ambayo inaruhusu kuwasiliana moja kwa moja au mtandaoni au ujanibishaji wa mtu. Katika muktadha huu panarejelewa zaidi taarifa yoyote kuhusu mtoto na maelezo ya kikosi chake ambayo yanakusanywa mtandaoni na watoa huduma wa mtandao, ikiwemo vidude vya kuchezea vilivyounganishwa na Mtandao wa mambo na mifumo mingine ya teknolojia iliyounganishwa.

***Faragha***

Faragha mara nyingi hupimwa kwa misingi ya usambazaji wa taarifa za kibinafsi mtandaoni, kuchapisha maelezo ya kibinafsi katika mitandao ya kijamii, kusambaza taarifa kwa watu unaofahamiana nao mtandaoni, kutumia mipangilio ya faragha, kufichulia marafiki nenosiri, kuwa na wasiwasi kuhusu faragha. [95]

***Kutuma jumbe za ngono***

Kutuma ujumbe wa ngono kwa kawaida hufafanuliwa kama kutuma, kupokea au kubadilishana maudhui ya ngono yaliyotayarishwa binafsi zikiwemo picha, ujumbe au video kupitia simu za mkononi na/au Mtandao. [96] Uundaji, usambazaji na umiliki wa picha za ngono

---

[94] UNICEF and ITU (2015), *Guidelines for Industry on Child Online Protectio*n, *https://www.itu.int/en/cop/Documents/bD_Broch_INDUSTRY_0909.pdf* .

[95] US Federal Trade Commission (1998), *Children's Online Privacy Protection Act*, *https://www.ecfr.gov/cgi-bin/text-idx?SID=4939e77c77a1a1a08c1cbf905fc4b409&node=16%3A1.0.1.3.36&rgn=div5*.

[96] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*,

za watoto ni kinyume cha sheria katika nchi nyingi. Ikiwa picha za ngono za watoto zimefichuliwa, watu wazima hawapaswi kuzitazama. Kusambaza picha za ngono na mtu mzima na mtoto daima ni kitendo cha uhalifu na kwamba madhara yanaweza kukumba watoto. Kuripoti na hatua za kuondoa picha zinazosambazwa huenda zikahitajika.

***Kulazimisha ngono kwa njia ya vitisho kutishia watoto ili kushiriki ngono nao***

Huku ni "kuharibu sifa ya mtu kwa kutumia picha alizojitengenezea mtu huyo ili kumlazimisha kushiriki naye ngono, pesa au manufaa mengine kutoka kwake chini ya tishio la kusambaza picha hizo bila idhini ya mtu huyo(k.m. kutuma picha kwenye mitandao ya kijamii)". [97]

***Mtandao wa Mambo***

Mtandao wa Mambo unawakilisha hatua inayofuata katika uundaji wa jamii iliyounganishwa kidijitali na uchumi, ambapo vitu na watu wameunganishwa kupitia mitandao ya mawasiliano na kusimulia hali zao na/au mazingira yanayowazunguka kidijitali. [98]

***URL***

Urefu wa herufi hizi ni 'uniform resource locator', anwani ya ukurasa wa Mtandao. [99]

***Uhalisia pepe***

Uhalisia pepe ni matumizi ya teknolojia ya kompyuta ili kuunda ulimwengu wenye mwingiliano wa pande tatu ambamo watu wana hisia za uwepo wa wawasiliani wao kihalisia. [100]

**WI-FI**

Wi-Fi (Wireless Fidelity) ni mkusanyiko wa viwango vya kiufundi vinavyowezesha utumaji wa data kupitia mitandao isiyotumia waya. [101]

---

*http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf*

[97] Terminology and Semantics (2016), *Luxembourg Terminology Guidelines for the Protection of Children from Sexual Exploitation and Sexual Abuse*, *http://luxembourgguidelines.org/wp-content/uploads/2017/06/Terminology-guidelines-396922-EN.pdf*

[98] Ntantko (2013), *The Internet of Things, Digital Single Market*, *https://ec.europa.eu/digital-single-market/en/internet-of-things*.

[99] UNICEF and ITU (2015), *Guidelines for Industry on Child Online Protection*, *https://www.itu.int/en/cop/Documents/bD_Broch_INDUSTRY_0909.pdf*.

[100] NASA (date?), *Virtual Reality*, online under: *https://www.nas.nasa.gov/Software/VWT/vr.html*.

[101] US Federal Trade Commission (1998), *Children's Online Privacy Protection Act*, *https://www.ecfr.gov/cgi-bin/text-idx?SID=4939e77c77a1a1a08c1cbf905fc4b409&node=16%3A1.0.1.3.36&rgn=div5.*

# African Telecommunications Union

CA Centre, Waiyaki Way

P. O Box 35282 – 00200 Nairobi, Kenya

Tel: +254 722 203132

Email: sg@atuuat.africa

Website: www.atuuat.africa

*****